




MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA



JARIDA LA HALI YA HEWA KILIMO

Na. 19. Msimu wa kilimo 2019/2020

Tathmini Aprili 1-10, 2020 na matazamio kwa kipindi cha Aprili 11-20, 2020

Muhtasari


- Mvua zinazoendelea kunyesha katika maeneo mengi ya nchi zitasaidia katika ukuaji wa mazao.
- Unyevunyevu uliokithiri unaweza kuathiri mazao hasusan yaliyopo mabondeni, wakulima wanashauriwa kutumia mbinu bora za uvunaji, ukaushaji na uhifadhi wa mazao.
- Wakulima, wafugaji na wavuvi wanashauriwa kupata ushauri wa maafisa ugani na kutumia taarifa za hali ya hewa katika shughuli zao za kila siku.

MIFUMO YA HALI YA HEWA KATIKA KIPINDI CHA APRILI 1-10, 2020

Katika dikadi hii, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kaskazini mwa dunia (Azore na Siberia) ilipungua nguvu wakati ile iliyopo kusini (St. Helena na Mascarene) iliimarika. Hali hii ilipelekea kuusukuma ukanda wa mvua kuelekea kaskazini mwa nchi. Uwepo wa Joto la bahari la juu ya wastani katika eneo la kusini magharibi mwa bahari ya Hindi (pwani ya Madagascar) lilisababisha kutokea kwa migandamizo midogo ya hewa. Katika eneo la kusini mashariki mwa bahari ya Atlantiki (karibu na pwani ya Angola) kulikuwa na joto la bahari la chini ya wastani na kupelekea kuwa na mchango mkubwa katika kuleta upepo wenye unyevunyevu kutoka misitu ya Congo kuelekea kwenye baadhi ya maeneo ya nchi. Uwepo wa migandamizo midogo ya hewa na joto la chini ya wastani kusini mashariki mwa bahari ya Atlantiki kulikua na mchango mkubwa wa mvua kwa baadhi ya maeneo nchini.

MWENENDO WA MVUA KATIKA KIPINDI CHA APRILI 1-11, 2020

Maeneo mengi ya nchi yamepata mvua kati ya 10 mm hadi 200 mm. Kiasi cha juu cha zaidi ya 200 mm kimerekodiwa katika mkoa wa Katavi. Hata hivyo, maeneo ya mikoa ya Lindi, Mtwara, Ruvuma, Iringa kaskazini, Dodoma, Singida na Mbeya yamepata kiasi cha mvua cha chini ya 10 mm, kama inavyoonekana katika kielelezo.



Kielelezo : Kiasi cha mvua katika kipindi cha Aprili 1-10, 2020

TATHMINI YA HALI YA KILIMO KATIKA KIPINDI CHA APRILI 1-10, 2020

Mvua zinazoendelea kunyesha katika maeneo mengi ya nchi zilisaidia katika ukuaji wa mazao. Zao la mahindi katika maeneo mengi yanayopata msimu wa mvua mara moja kwa mwaka lipo katika hatua ya kukomaa na uvunaji. Wakulima katika mikoa ya Iringa, Njombe, Singida na Ruvuma walikuwa wanaendelea na uvunaji wa maharagwe. Kwa upande mwingine, maeneo yanayopata mvua mara mbili kwa mwaka, wakulima waliendelea na shughuli za utunzaji wa mashamba na upandaji. Aidha, maeneo machache ya ukanda wa

pwani ya kaskazini (Morogoro, Tanga, na visiwa vya Pemba, na Unguja) zao la mpunga lilikuwa katika hatua ya kutoa maua.

HALI YA MAJI ILIVYOKUWA KATIKA KIPINDI CHA APRILI 1-10, 2020

Kiwango cha maji katika mabwawa na kutiririka kwa maji katika mito vimeongezeka katika maeneo mengi ya nchi kutokana na mvua za *Masika* na Musimu zinazoendelea.

MIFUMO YA HALI YA HEWA INAVYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA APRILI 11-20, 2020

Katika dikadi hii mifumo ya migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kaskazini mwa dunia inatarajiwa kuendelea kupungua nguvu, wakati ile iliyopo kusini inatarajiwa kuendelea kuongezeka nguvu. Hali hii itasababisha ukanda wa mvua kuwa kaskazini mwa nchi. Joto la bahari la juu ya wastani linatarajiwa kuwepo katika eneo la kusini magharibi mwa Bahari ya Hindi (kusini mashariki mwa Bahari ya Atlantiki, karibu na pwani ya Angola) na kusababisha vipindi vya migandamizo midogo ya hewa kusini magharibi mwa Bahari ya Hindi. Hali hii itaimarisha upepo unaovuma kutoka magharibi (katika misitu ya Congo) kuelekea maeneo ya nchi yetu, hivyo kuwa na mchango mkubwa katika kuimarisha mifumo ya mvua katika baadhi ya maeneo ya magharibi, ukanda wa Ziwa Victoria pamoja na kaskazini mwa nchi.

HALI YA HEWA INAVYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA APRILI 11-20, 2020.

Maeneo ya kanda ya Ziwa Viktoria (mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Simiyu na Mara) na magharibi mwa nchi (mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora) yanatarajiwa kupata mvua za wastani katika baadhi ya maeneo hususan nusu ya pili ya dekad.

Pwani ya kaskazini (mkoa wa Tanga, kaskazini mwa mkoa wa Morogoro, mikoa ya Pwani na Dar es Salaam pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba) kunatarajiwa kupata mvua za wastani katika baadhi ya maeneo.

Nyanda za juu kusini magharibi (mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya,

Njombe na Iringa), kanda ya kusini (mkoa wa Ruvuma na kusini mwa mkoa wa Morogoro) na nyanda za juu kaskazini mashariki (mikoa ya Arusha, Manyara na Kilimanjaro) yanatarajiwa kupata mvua za wastani katika maeneo machache.

Kanda ya kati (mikoa ya Dodoma na Singida) na pwani ya kusini (mikoa ya Mtwara na Lindi) yanatarajiwa kupata mvua nyepesi katika maeneo machache.

HALI YA HEWA KILIMO INAVYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA APRILI 11-20, 2020

Mvua zinazotarajiwa katika maeneo mengi yanayopata misimu miwili ya mvua kwa mwaka zitasaidia ongezeko la unyenyevu kwenye udongo na kuimarisha ukuaji wa mazao. Ongezeko hili, linaweza kuathiri mazao yaliyopo mabondeni hususan katika mikoa ya Dodoma, Singida, Dar es Salaam, Lindi, Mtwara, Ruvuma, Morogoro, Rukwa na Mbeya ambako kumeripotiwa unyenyevu uliokithiri na mafuriko. Wakulima wanashauriwa kuchukua hatua stahiki na kutumia njia bora za kilimo ili kuepusha athari za unyenyevu uliokithiri. Wakulima, wafugaji na wavuvi wanashauriwa kupata ushauri wa maafisa ugani katika maeneo yao.

HALI YA MAJI INAVYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA APRILI 11-20, 2020

Kina cha maji katika mabwawa na mtiririko wa maji kwenye mito vinatarajiwa kuendelea kuongezeka katika maeneo mengi ya nchi. Hata hivyo, watumiaji wa maji wanashauriwa kuendelea kuyatumia kwa uangalifu na kuchukua tahadhari juu ya athari zitokanazo na mafuriko.

Jarida limetayarishwa na:

Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania

Ghorofa ya 3-Ubungo Plaza – 388 Barabara ya Morogoro,

S.L.P 3056; 16102 Dar es Salaam, Simu. 255-(0) 22 – 2460706-8; Nukushi: 255 - (0) 22 – 2460718 ; Barua pepe: (1) met@meteo.go.tz (2) agromet@meteo.go.tz; Tovuti:

www.meteo.go.tz, -Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania